Tafakuri ya Miaka 50 ya Uhuru

Issa Shivji
Profesa wa Kigoda cha Taaluma cha Mwalimu Nyerere
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Ushangiliaji na upondaji

Maadhimisho ya miaka 50 ya Uhuru wa Tanganyika ni wakati mwafaka wa kutafakari kwa kina tulipotoka, tulipo na kwa nini tupo hapa tulipo. Tafakuri hii itakuwa ya namna tofauti tofauti kutegemeana nani na kwa maslahi gani anashangilia au anaponda miaka 50 ya uhuru. Watakuwapo washangiliaji: Tumeendelea – angalieni mabarabara zetu za lami, maghorofa yetu marefu, shule tulizozijenga na magari tuliyonunua. Ndivyo watakavyojigamba watawala. Watataja na kuorodhesha mafanikio.

Watakuwapo, hususun, wanasiasa-wapinzani, au watawala-watarajiwa watakaoponda – shule zenu hazina walimu na elimu inayotolewa haikidhi mahitaji ya dunia ya utandawazi. Umaskini umezidi, angalia watoto wanaolala mitaani, na maskini wanaoombaomba mijini. Miaka hamsini ya uhuru na bado hatuna demokrasia ya kutosha. Wapinzani watadai wanateswa na hawapewi uhuru wa kutosha, uchaguzi unachakachuliwa, na utajiri wa nchi unafisidiwa.

Katika mabishano haya ya kisiasa na kwa masilahi ya kisiasa, kuna chembe za ukweli pande zote, lakini ukweli huu utapotea katika malumbano ya kisiasa yasiyogusa matakwa ya wananchi wavujajasho. Na, kama ilivyo hulka ya wanasiasa popote pale, ukweli utapindishwa, uongo utashamirishwa. Uchambuzi utabezwa, propaganda zitaenezwa.

Wananchi watazamaji

Kwa jumla, wananchi wenyewe, watakuwa wasikilizaji na watazamaji. Hawataalikwa au kuhudhuria mahafali mengi tu ya kusheherekea miaka 50. Lakini wataruhusiwa kutembelea maonyesho huko Mnazi Moja yalioandaliwa na wizara na idara za serikali zikitambia maendeleo ya idara zao. Watoto watafurahia vipeperushi vya aina na aina, ingawa wangetamani zaidi fuluna na kofia maalum watakazovaa waonyeshaji wa wizara, wakiwa wana kula kuku na chipsi na kkunywa soda kama kifutajasho. Wananchi watafuta jasho lao kwa vipeperushi!

Hohehahe watajikusanya katika mikutano na maandamano ya wapinzani wakivutiwa na muziki na ngoma. Wanasiasa-wapinzani watatumia fursa hizi kutafuta umaarufu na wafuasi ili waingie madarakani katika uchaguzi ujao. Basi, tutashuhudia na tumeshaanza kushuhudia hayo yote na mengine mengi tukifika kilele cha Uhuru wetu tarehe 9 Desemba.

Baada ya kilele tutarejea maisha ya kawaida, kila moja akiendelea na shughuli zake – walionacho wakiendelea kuishi maisha ya anasa, wasionacho wakiendelea kujikamua kila tone la jasho lao ilimradi wapate angalau donge la dona na kitoweo cha sukuma-wiki.

Uchambuzi wa kina

Kama kweli tunataka kujua, kuelewa na kutathmini ukweli wa mambo, na hali halisi ya jamii na taifa letu, hatuna budi tuzingatie mambo mawili ya msingi. Mosi, wachambuzi waamue makasudi kabisa na kuweka wazi wanachotetea katika tathmini zao za miaka 50: je, ni kwa maslahi ya nani, wavujajasho au wavunajasho? Tumechoka na wababaishaji wanaojifanya wasomi waliobobea au wataalamu wakitetea maslahi yao au ya tabaka lao la walalahai na walalaheri huku wakijidai kwamba uchambuzi wao ni wa kisayansi. Pili, tuzingatie kwamba hatuwezi kuchukua miaka 50 kama kipindi kimoja cha tarehe za kalenda bali ni historia ya mapambano ya kijamii na imekuwa na vipindi mbalimbali pamoja na mwelekeo na mtazamo wake mahsusi.

Tathmini ya miaka 50

Kwa upande wangu, ningependa kusema awali ya yote kwamba nitajaribu kufanya tathmini ya miaka 50 kwa msimamo wa walalahoi. Mafanikio na makosa yatapimwa kwa vigezo vya matakwa na mtazamo wa matabaka ya wavujajasho.

Enzi ya kizalendo

Historia yetu ya nusu karne tunaweza tukaigawa kwa vipindi viwili: miaka 25 ya mwanzo (1961-1985) ambayo tunaweza tukaiita **enzi ya kizalendo** na miaka 25 iliyofuata (1986-2005) ambayo tunaweza tukaibatiza kama **enzi ya uliberali-mamboleo**. Kilele cha enzi ya kizalendo bila shaka ni miaka 10 ya Azimio la Arusha, yaani, 1967-1977. Na kilele cha enzi ya uliberali-mamboleo ni miaka 10 ya utawala wa Mheshimiwa Mkapa, 1995-2005. Kama Mwalimu Nyerere ni muasisi wa uzalendo nchini basi

Mheshimiwa Mkapa ni muasisi wa uliberali-mamboleo, mara nyingine huitwa enzi ya utandawazi.

Vipindi vingine vya katikati ni vipindi vya mpito.

Uchumi kilema

Baada ya 1977, na hasa baada ya vita vya Uganda mnamo mwaka wa 1979, uchumi wetu na hata siasa zetu zikaingia kwenye kipindi kigumu cha zahama (crisis). Miaka mitano ya mwisho ya Mwalimu ilikuwa ya misukosuko kwa sababu mbalimbali za ndani na nje. Pamoja na sera za kimaendeleo wakati wa enzi ya Mwalimu, ukweli ni kwamba hatukufanikiwa kujikomboa kutokana na uchumi wa kibepari wa kimataifa, yaani, ubeberu. Tukaendelea kuwa na uchumi tegemezi. Katika ujenzi wa mfumo wa kijamaa makosa yalifanyika, mengine Mwalimu mwenyewe alikiri katika hotuba yake ya miaka kumi ya Azimio. Alitaja kinagaubaga kwamba tulikosea kufuta serikali za mitaa chini ya sera ya madaraka mikoani iliyobuniwa na kampuni moja ya Kimarekani, Mackenzi. Ukweli ni kwamba badala ya kupanua demokrasia, madaraka mikoani yakapeleka utawala wa kirasimu karibu zaidi na wananchi; yakawa 'madaraka mikononi' badala ya 'madaraka mikoani'.

Pili, tulikosea kuvifuta vyombo vya ushirika vya wakulima wenyewe na badala yake tukaweka Mamlaka za Serikali ambazo zikawajengea wamangimeza (au vibwenyeye wa kirasimu kama sisi vijana tulivyokuwa tukiwaita siku zile) uwezo wa kuwanyonya wakulima na kujilimbikizia marupurupu chungu nzima wakiishi maisha ya anasa. Tatu, mwelekeo wa kujenga viwanda vya kuzalisha bidhaa za anasa pia ukatufanya tukose uwezo wa kujenga viwanda vya msingi vya kuzalisha zana za kilimo na uzalishaji kwa jumla. Ingawa hatunabudi tukiri kwamba kulikuwa na hatua za dhati kujenga viwanda vya kuzalisha mahitaji ya wananchi wa kawaida, kwa mfano, viwanda vya kuzalisha nguo kama Urafiki, kiwanda cha kuzalisha zana za kilimo kama Ubungo, viwanda vya kuzalisha mafuta ya kupikia, n.k.

Pamoja na haya yote, na mafanikio katika kutoa huduma za kijamii kama elimu, afya, maji n.k., ukweli unabaki palepale kwamba uchumi wetu kwa jumla ulikuwa bado na sifa za uchumi tegemezi. Na hili Mwalimu mwenyewe alikiri baada ya kung'atuka. Mnamo

mwaka wa 1989 akizungumza na viongozi wa serikali na mashirika ya umma, akasema, na ninamnukuu:

Sifa ya kwanza ya uchumi wetu ni duni, hii sifa ya uduni ni mbaya lakini si mbaya sana hii, inawezekana ikawa ni kama la kawaida. Kwa nini? Kwa sababu kama kuna duni kule ni uchumi ulioko nyuma kama maana yake ingekuwa uchumi mchanga, uchumi ambao haujakomaa. ... ...
Kwa maana hiyo, uduni huo ni uchumi uko nyuma isingekuwa mbaya kama ingekuwa sifa hiyo peke yake tu tungeweza kuutilia mbolea uchumi ule ukabadilika.

Lakini uchumi huu una sifa ya pili, ni uchumi tegemezi. Ni uchumi unaotegemea Kaskazini, tena sifa ile ya kutegemea inaupa ugonjwa. Kwa hiyo, utegemeaji ule ni kama maradhi; maradhi hayatokani na uduni peke yake, maradhi, hasa ya uchumi wetu ni ule utegemezi wake ... ... Ni ugonjwa. Ni kilema. Ni uchumi kilema. ... ...

Kwa hiyo, kama unatazama magwaride ya kijeshi, kama unatazama viwanja vya ndege, sisi hatuna ndege nyingi sana, lakini hata Dar es Salaam nenda uone ndege ziko pale. Hata Dar es Salaam utakuta ndege pale. Magwaride ya majeshi, viwanja vya ndege, hata nchi zenyewe ziwe zina mali nyingi kama vile nchi zenye uwezo wa kutoa mafuta, utakuta zimejaa tele viwanja vya madege makubwa makubwa ya kila aina.

Mabarabara yetu katika nchi za Kusini yamejaa magari tele, ikiwa ni pamoja na Dar es Salaam. Kwa baadhi ya nchi zingine, hata bidhaa madukani, maduka yamejaa tele – zimetengenezwa wapi? Yote hayo kama magwaride, kama ni viwanja vya ndege, kama magari, kama ni bidhaa madukani nasema kwa baadhi ya nchi fulani fulani hata kama ni Coca-Cola ni maonyesho, ni magwaride ya utegemezi kote katika nchi zetu.

Kwa Coca-Cola, kwa sababu Marekani wao wana nguvu sana kwa Coca-Cola, Marekani sasa anataka wote tuwe ni wanywa Coca-cola. Ndugu Mengi mkipenda msipende, mtatuuzia tu Coca-Cola basi Coca-Cola inauzwa tu.

Sasa uchumi wetu basi ni uchumi tegemezi. Uchumi wa nchi zetu hizi zote una sifa hizo mbili. Hili tatizo letu kubwa la msingi. Uchumi wetu ni uchumi duni, lakini uduni peke yake si kitu sana, lakini tatizo kubwa kabisa kabisa ni uchumi tegemezi.

Kwa hiyo tunajivunia ule ugonjwa… tunajivunia ule ugonjwa wala hatuuonei haya… unaparedi silaha za wakubwa, unaparedi madege ya wakubwa, unaparedi bidhaa za wakubwa, unaparedi ma-Coca-Cola ya wakubwa na unajivuna tu, unasema sisi tumeendelea. Ukimwambia umeendelea kwa nini atakwambia njoo uone barabara yetu.I (Chanzo: Mzalendo, 21/05/1989*)*

Katika hili, Mwalimu bila kutumia neno lenyewe, anasema kwa uwazi kwamba uchumi wetu ni uchumi tegemezi ambao unategemea nchi za kibeberu. Na pia kwa kuainisha

uchumi wetu hivi anakiri kwamba licha ya hatua zilizochukuliwa wakati wa utawala wake, bado hatukufanikiwa kuukomboa uchumi wetu kutoka katika maradhi ya utegemezi. Na vidudu vya ugonjwa huu ndivyo vikalipuka kwa kasi mnamo miaka ya 1980 na kuzaa kipindi cha zahama za uchumi.

Kama nilivyosema kipindi cha mwisho cha Mwalimu kilikuwa kigumu. Bidhaa za lazima zilikuwa hazipatikani, uwezo wa uchumi kulipia madeni ulipungua sana, uzalishaji ukadhoofika, walanguzi wakaenea, foleni zikawa ndefu, serikali ikaanza kupoteza uhalali na umaarufu wake, hongo ikashamiri. Na vuguvugu la wapinga ujamaa likaanza kujitokeza kwa uwazi zaidi. Nchi za kibeberu na taasisi zake kama Shirika la Fedha na Benki ya Dunia wakaanza kutuwekea ugumu na masharti.

CCM chenyewe kikafanya uchambuzi na tathmini ya kipindi hiki katika Mwongozo wa 1981. Pamoja na mambo mengine Mwongozo ukaeleza waziwazi kwamba chini ya mvavuli wa mashirika ya umma, kilichotokea ni ujenzi wa tabaka la vibwenyeye wa kirasimu (bureaucratic bourgeoisie) na sasa walianza kujitokeza kupindua Ujamaa na Kujitegemea, wakishirikiana na nchi za kibeberu zikiongozwa na Ronald Reagan (rais wa zamani wa Marekani) na Margaret Thatcher (waziri mkuu wa zamani wa Uingereza) ambao walikuwa vinara wa utandawazi na uliberali-mamboleo.

Utandawizi wa utandawazi

Utandawazi haukuwa jambo jingine isipokuwa ni jina lingine tu la ubeberu. Na sera za uliberali-mamboleo hazikuwa zingine isipokuwa tu kumeza zaidi nchi za Afrika katika mfumo wa ubepari wa kimataifa na kuendelea kutunyonya. Kwa upande wetu, wale waliokumbatia sera hizi wakawa wapigadebe wa akina Reagan na Thatcher na tukaingia kwenye kipindi kingine cha utegemezi, au ukoloni mamboleo, isipokuwa safari hii bila kipingamizi, ni kwa hiari yetu, au labda kwa sahihi zaidi, ni kwa utashi na matakwa ya vibwenyeye wetu.

Ndio maana, pamoja na uchambuzi sahihi wa Mwongozo, CCM ikashindwa kusimamia mtazamo wake wa Kijamaa. Mwalimu akang'atuka. Tukaingia kwenye enzi ya Mzee Ruksa, ambayo serikali yake ikaanza, hatua kwa hatua, kufungua milango ya biashara ya nje na ndani na kulegeza masharti ya kudhibiti uchumi. Katika kipindi cha pili cha Mzee Mwinyi, mchakato wa kubinafsisha mashirika ya umma ukaanza kwa kusitasita, hasa

kwa sababu Mwalimu aliendelea kusoakosoa sera za uliberali-mamboleo. Kwa hivyo, urais wa Mwinyi ni kipindi cha mpito kati ya uzalendo na uliberali-mamboleo.

Awamu ya tatu ya Mheshimiwa Benjamin Mkapa ndiyo haswa ilikuwa kilele cha sera na mfumo wa uliberali-mamboleo. NBC, benki peke yake ya kibiashara nchini, ikabinafsishwa kwa kampuni moja ya makaburu kutoka Afrika ya Kusini kwa bei poa. Sekta ya fedha ikafunguliwa milango bila kudhibitiwa. Mashirika mengine, hata yale yaliokuwa yanatoa faida na kulipa kodi kwa serikali, kama kiwanda cha bia na sigara, yakauzwa. Viwanda vingine, kama TIPER chaa kusafishi mafuta na NMC chaa kuhifadhi nafaka, ambavyo kwa kiasi fulani vilikuwa kinga chetu dhidi ya mfumuko wa bei ya bidhaa muhimu katika soko la kimataifa, vikabinafsishwa. Mnunuzi wa TIPER akangoa mitambo na kufanya jengo lenyewe kuwa ghala wakati mafuta yenyewe yakitoka nje kutoka makampuni dada. Msukumo wa ubepari ni mmoja tu - kuchuma faida na ndio unaongoza uzalishaji na usambazaji wa bidhaa, hata bidhaa muhimu kwa mahitaji ya binadamu, kama chakula na nafaka. Kwa hivyo, mmliki wa NMC akaanza kuzalisha na kuuza vyakula kwa kufuata soko lenye bei kubwa bila kujali mahitaji ya wananchi. Serikali, ambayo ilikumbatia soko huria, ikajikuta haina uwezo wa kudhibiti bei za bidhaa muhimu, pamoja na chakula, nafaka na mafuta. Hivi majuzi serikali ilipojaribu kupanga bei ya mafuta, wenye makampuni ya mafuta wakagoma kiasi cha kuidhalalisha serikali machoni mwa wananchi wake. Tusilalamike, ndio ukweli wa mfumo tuliochagua.

Mambo mengi muhimu na ya msingi katika mageuzi ya uchumi yalifanyika chini ya awamu ya tatu. Sheria za Ardhi zilizotoa mwanya kwa waporaji wa ndani na nje zikapitishwa mnamo mwaka 1998 na baadae zikarekebishwa mwaka wa 2004 kutokana na shinikizo la mabenki. Marekebisho ya 2004 kwa mara ya kwanza yakafanya ardhi tupu kuwa na thamani na kuweza kuuzwa. Sera ya mchumi mmoja wa mrengo wa kulia, Bwana Hernando de Soto, ambaye anasisitiza urasimishaji wa mali ya wanyonge ili kujenga uchumi imara wa kibepari, ikakumbatiwa na Mheshemiwa Mkapa. Ikabatizwa jina MKURABITA, yaani, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania. Urasimishaji wa biasahara ni kiini macho; ukweli ni kurasimisha ardhi, ambayo ni rasilimali ya msingi ya wakulima na wafugaji. Kurasimisha umiliki wa ardhi maana yake halisi ni kuwezesha ardhi kuuzwa sokoni kama shati. Mpango kama huo popote pale ulipojaribiwa katika bara la Afrika unaonyesha kwamba hatma yake ni wazalishaji

wadogo vijijini kupoteza ardhi yao na ardhi kulimbikizwa mikononi mwa wawekezaji na waporaji wa ndani, lakini zaidi, mwa makampuni ya kimataifa kutoka nchi za kibepari.

Mnamo mwaka wa 1998 Sheria ya Madini ikapitishwa ambayo kisheria ikawawezesha wawekezaji wa migodi kuchuma faida bila kulipa kodi na mambo mengine ambayo tunayalalamikia sana siku hizi. Sheria ya kudhibiti kodi ya nyumba iliyopitishwa mara baada ya uhuru mnamo mwaka wa 1962 kulinda wapangaji ikafutwa. Mwenye nyumba sasa ana uhuru wa kupanga kodi pamoja na kumfukuza mpangaji wake bila kizuizi chochote cha kisheria. Sheria ya Shirika la Nyumba ambalo lengo lilikuwa kuwapatia wananchi makazi likarekebishwa na kupewa uhuru wa kujiendesha kibiashara bila kujali mahitaji ya wananchi. Nyumba za serikali zikauzwa kwa viongozi wa kisiasa na watumishi wa ngazi za juu.

Sheria za Kazi zilizopitishwa baada ya uhuru zikiwa na lengo la kuwa na tabaka la kudumu la wafanyakazi badala ya wafanyakazi wa mzunguko au manamba kwa kuwaongezea mishahara na kuweka kima cha chini zilifutwa. Sheria ya kiinua mgongo pia ikarekebishwa. Sheria mpya za kazi kukidhi soko huria na kuwapa uhuru zaidi waajiri kuajiri na kuwafukuza waajiriwa wao zilizoandikwa na mtaalam-mshauri kutoka Afrika ya Kusini akifadhiliwa na serikali ya Demnmark zikapitishwa.

Kwa ufupi basi mafanikio karibu yote ya kipindi cha uzalendo yakapinduliwa. Uliberali-mamboleo au utandawazi uliotangazwa na kusimamiwa na nchi za kibeberu, taasisi zao za kimataifa na wanansiasa-uchwara wa ndani ulikuwa kinyume cha uzalendo, kiuchumi, kitikadi, kisiasa na kijamii.

Tunavuna matunda machungu ya utandawazi

Leo katika awamu ya nne tunazungumzia na kuyalalamikia mambo mengi tu. Jamii yetu imepasuka vibaya. Leo hii tuna jamii yenye matabaka ya walionacho na wasionacho. Utajiri wa wachache ni wa kupindukia kama ulivyo umaskini wa wengi. Uchumi, tunaambiwa, unakua; lakini umaskini unakuwa maradufu. Kati ya 2001 na 2007, idadi ya maskini, yaani wenye kipato chini ya dola 2 za Marekani, imeongezeka kuwa watu milioni 4.5. Ajira ni finyu. Karibu robo tatu ya wananchi hutegemea kilimo lakini kilimo huchangia robo tu ya pato la taifa. Ajira katika sekta ya viwanda ni chini ya watu laki moja na haijaongezeka kati ya 2001 na 2007. Lakini ajira katika sekta isiyorasmi - yaani

wachuuzi na wamachinga - imeongezeka kwa asilimia zaidi ya 90. Yaani wanaotegemea sekta isiyorasmi, ni mara 17 ya ajira rasmi katika sekta ya viwanda. Ajira ya akinamama wafanyao kazi majumbani kwa watu imeongezeka kwa asilimia 33. Hayo ni dalili za ugonjwa wa uchumi; sio jambo la kujivunia.

Uwekezaji, ambao tunaambiwa, ni gurudumu la maendeleo umekua. Wastani wa uwekezaji kutoka nchi za nje kila mwaka kati ya 1997 na 2009 ni dola za Marekani milioni 439 lakini zaidi ya asilimia 95 ni katika sekta ya madini, sekta ambayo unachimba tu utajiri wa nchi na kusafirisha nje bila kuchangia katika kuendeleza uchumi wa ndani. Kwa mfano, mchango wa madini kwa mauzo ya nje ni asilimia 39, lakini machango wa sekta ya madini kwa pato la taifa ni chini ya asilimia 3! Mbaya zaidi uwekezaji wa dola milioni 439 kila mwaka umezaa ajira ya watu elfu saba tu, yaani ajira katika kazi za nyumbani ni mara kumi ya ajira migodini. Wakati huo huo wanaoingia katika soko ya ajira kila mwaka ni zaidi ya laki nane.

Sifa hizi nilizotaja ni sifa sio tu ya uchumi tegemezi, kama alivyoainisha Mwalimu, lakini ni uchumi uchwara, kwa maana ya kwamba uchumi usioendelevu, uchumi usio na matumaini ya kuwaletea maendeleo walio wengi.

Ubepari-uchwara huzaa siasa-uchwara

Tuwe wawazi. Mbegu za mfumo uliotufikisha hapo tulipo zilipandwa katika awamu ya tatu. Walichofanya wanamtandao ni kupalilia tu shamba. Na sasa tunavuna "matunda" machungu ya mfumo wa ubepari-uchwara.

Uchumi-uchwara huzaa siasa-uchwara. Siasa-uchwara huendeshwa kwa mabavu, vitisho, ulaghai na malumbano kwa sababu hukosa uhalali katika macho ya wananchi waliowengi. Tusilalamike na tusiingizwe katika malumbano ya wanasiasa bila kuelewa na kujadili chanzo cha udhaifu wetu kisiasa na uduni wetu kiuchumi. Tutafakari na baada ya kutafakari tujiulize: Nani atatukomboa - wawekezaji, wafadhili, viongozi au wananchi wavujajasho wakiongozwa na viongozi wao wenyewe.

Tujiulize: Katika jamii yetu ya leo nani anafaidika na nani anaathirika na mfumo tulionao? Je, wanaochuma kutokana na udhaifu wetu watatuongozo kujikomboa? Sina majibu; nina maswali tu. Majibu yatapatikana katika tafakuri, mijadala na mapambano ya

wananchi walalahoi wenyewe. Sisi wengine, wasomi na wanazuoni, wazalendo na wakereketwa, tuchangie katika kuelewa hali halisi na kuuliza maswali sahihi bila kujali maslahi yetu binafsi. Tuache kujipendekeza; tuache kuwa na ndoto za kuwa mawaziri.

Kwa mwanazuoni au msomi, kujipendekeza kwa watawala au watawala-watarajiwa ni usaliti wa umma.

© *Issa Shivji*